**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**
S.L.P. 138 SAME

**Kumb.Na.**SDC/S.30/23VOL/1 02 Mei, 2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same amepokea Kibali cha Ajira Mpya kutoka kwa Katibu Mkuu – ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia baru ayenye **Kumb. Na. FA.228/613/01F/072 ya tarehe 10.03.2025.** Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi tajwa hapo chini.

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 1)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi;
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari;
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;
vi. Kufanya usafi wa gari;
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa au kujiandikisha.
ii. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) awe na Lesseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari **‘Basic Driving Course”** yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA au NIT) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

iv. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA TGS B

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45;

ii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika;

iii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa kilichodhibitishwa na Mwanasheria/Wakili;

iv. Maombi yote yaambatane na cheti cha taaluma na nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho.

- Certificates;
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI;
- Vyeti vya kitaaluma (professional Certificates)
- Picha moja ‘pasport size’ ya hivi karibuni;

v. Testimonials ‘provisional results’ results slip’ kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa ***HAVITAKUBALIWA.***

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

vii. Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa / kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi;

viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria;

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **31 Novemba, 2010.**

x. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni ***tarehe 11 Mei, 2025.***

xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **hayatafikiriwa;**

xii. Mwombaji atatakiwa kuambatisha nakala ya kitambulisho cha uraia (NIDA) au namba ya NIDA kama hana kitambulisho;

xiii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa Ajira Aina ya ulemavu walionao;

xiv. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Same,
S.L.P 38,
**SAME**

xv. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielectroniki wa Ajira Recruitment Portal kupitia anuani ifuatayo; *https://portal.ajira.go.tz* (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuto ya Seckretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘Recruitment Portal’)

xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.

***LIMETOLEWA NA:***

**MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA SAME**